

# Mambo 7 wazazi wanapaswa kufahamu kuhusu chanjo ya COVID-19



## 1. Watoto wanahitaji kupewa chanjo.

COVID-19 ni hatari zaidi ikilinganishwa na hatari zinazowezekana kutokana na kupata chanjo. Watoto wengi zaidi wanapata athari mbaya, za kudumu kutokana na virusi na kulazwa hospitalini tunaposhuhudia aina mpya za virusi. COVID-19 sasa ni mojawapo ya vyanzo vikuu 10 vya vifo kwa vijana, na 1/3 ya vijana waliolazwa hospitalini walihitaji huduma za wagonjwa mahututi.<sup>1</sup>



## 2. Mchakato wa kuunda chanjo haukuharakishwa.

Wanasayansi wamekuwa wakishughulikia teknolojia hii kwa zaidi ya mwongo mmoja. Hakuna hatua za usalama zilizorukwa katika kuunda chanjo za COVID-19—ni kanuni za kawaida na urasimu pekee—na majaribio ya kimatibabu yalipitia hatua sawa na chanjo nyingine yoyote. Tunajua chanjo ni salama na zenye ufanisi kwa sababu mamia ya maelfu ya watu walijitolea kwa majaribio ya kimatibabu. Wanasayansi waliweza kuchunguza chanjo haraka—badala ya kusubiri miaka kadhaa kupata washiriki wa kutosha.



## 3. Athari nyepesi au za wastani ni kawaida.

Mtoto wako anaweza kuwa na dalili nyepesi au za wastani baada ya kupata chanjo, kama vile homa, maumivu ya misuli, maumivu ya kichwa, kuhisi uchovu, au wekundu karibu na eneo alilodungwa sindano. Hii ni kawaida baada ya chanjo yoyote, na inamaanisha mwili wako umeanza kuunda mwitikio wa kinga na unajifunza kupambana na ugonjwa. Athari kali na athari za mzio ni nadra. Uwezekano wako wa kuwa na hali ya kutishia maisha ya COVID-19 ni kubwa zaidi kuliko hatari yako ya kupata athari kali kutokana na chanjo.



## 4. Athari za muda mrefu, kama vile utasa au kuharibika kwa mimba, zina uwezekano mdogo.

Ukiangalia historia ya chanjo zote, karibu kila athari ya muda mrefu kutokana na chanjo hujitokeza kati ya siku 30-45 baada ya majaribio ya kimatibabu ya chanjo kumalizika. Ndiyo sababu FDA inahitaji muda wa kusubiri wa angalau siku 60 baada ya kumalizika kwa jaribio la kimatibabu kabla ya idhini ya matumizi ya dharura (EUA) kutolewa.

Maelfu ya wanawake wamepokea chanjo wakati walikuwa wajawazito au wamepata ujauzito baada ya kupata chanjo. Data inaonyesha kuwa chanjo za COVID-19 hazijasababisha utasa, kuharibika kwa mimba, au matatizo ya ujauzito au kujifungua kwa mama au mtoto. Hata hivyo, tumeshuhudia wanawake wengi wajawazito wakipata COVID-19 na wanakabiliwa na matatizo makubwa kutokana na virusi.

<sup>1</sup> [https://www.cdc.gov/mmwr/volumes/70/wr/mm7023e1.htm?s\\_cid=mm7023e1\\_w%20\[cdc.gov\]](https://www.cdc.gov/mmwr/volumes/70/wr/mm7023e1.htm?s_cid=mm7023e1_w%20[cdc.gov])



## 5. Chanjo ina ufanisi wa JUU.

Jaribio la kimatibabu lilionyesha chanjo ya COVID-19 ina ufanisi wa asilimia 100 katika kuingia watoto wenye umri wa miaka 12-15 dhidi ya virusi. Chanjo inafanya kazi dhidi ya aina tofauti za virusi, inazuia kuenea kwa watu wengine<sup>2</sup>, na inaweza kweli kuboresha mambo<sup>3</sup> kwa wale ambao wanakabiliwa na athari za muda mrefu za COVID-19. Kupata chanjo pia hufanya maradhi kuwa mepesi na mafupi kwa watu wachache sana ambao wanatambuliwa kuwa na maambukizi baada ya kupata chanjo.<sup>4</sup>



## 6. Hata kama mtoto wako tayari alikuwa na COVID-19, anapaswa kupata chanjo.

Mtoto wako anapaswa kupata chanjo, hata ikiwa hakuugua sana kutokana na virusi hapo awali. Uchunguzi unaonyesha chanjo hutoa kinga ya muda mrefu kuliko kinga ya asili (kinga kutokana na ugonjwa) na inalinda dhidi ya aina tofauti za virusi. Chanjo inaweza kumfanya mtoto wako asipate virusi tena.



## 7. Chanjo za mRNA za COVID-19 hazibadilishi DNA yako.

Kuna vitu **chanjo za mRNA HAIWEZI** kufanya<sup>5</sup>:

- mRNA haiwezi kurekebisha au kubadilisha DNA yako
- mRNA haiwezi hata kuingia kwenye sehemu ya seli zako ambapo DNA iko (inayoitwa kiini)
- mRNA haiwezi kujibadilisha na kuwa DNA

<sup>2</sup> <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/science/science-briefs/fully-vaccinated-people.html>

<sup>3</sup> <https://www.yalemedicine.org/news/vaccines-long-covid>

<sup>4</sup> <https://www.cdc.gov/media/releases/2021/p0607-mrna-reduce-risks.html>

<sup>5</sup> <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/different-vaccines/mrna.html>